**TAARIFA KWA UMMA:**

**MKUTANO WA TATU WA KIKOSI KAZI CHA MASUALA YA BIMA (TECHNICAL WORKING GROUP) ULIOFANYIKA TAREHE 23 MACHI 2023 JIJINI DAR ES SALAAM NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAENEO YA BIMA KWENYE MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA SEKTA YA FEDHA WA MIAKA KUMI (2020/21 – 2029/30).**

## UTANGULIZI

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) iliundwa kwa Sheria ya Bima Sura Na. 394 ("**Sheria ya Bima**") ikiwa chini ya usimamizi wa jumla wa Waziri wa Fedha na Mipango. TIRA imepewa jukumu la **kuratibu masuala yanayohusu bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Majukumu makuu ya Mamlaka ni kujenga na kuendeleza soko la bima jumuishi, soko lenye ufanisi, kusimamia haki, Soko salama, na himilivu kwa manufaa ya wakatabima na wanufaika wengine wa bima. Majukumu mahususi ya Mamlaka yapo katika maeneo makuu manne kama ifuatavyo:

i. **Kusajili na kutoa leseni kwa wasajiliwa wa Bima,**
ii. **Kusimamia sheria na utendaji wa watoa huduma za Bima,**
iii. **Kuwalinda walaji na wanufaika wa huduma na bidhaa za Bima** na
iv. **Kuendeleza Soko la Bima la Tanzania**.

## Utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (FSDMP) kupitia Kikosi Kazi cha Masuala ya Bima

Sekta ndogo ya bima ni moja ya sekta ndogo tano za Sekta ya fedha zinazowajibika kutekeleza FSDMP. Mpango huu ni wa Miaka 10 uliowekwa na Serikali kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ya fedha kwa kipindi cha 2020/21-2029/30. Sekta ndogo zingine zinazotekeleza FSDMP ni sekta ndogo ya benki; sekta ndogo ya masoko ya mitaji na dhamana; sekta ndogo ya kinga ya jamii; na sekta ndogo ya huduma ndogondogo za kifedha.

Ili kuratibu utekelezaji wa FSDMP, kila sekta ndogo ya fedha imejiwekea Mpango Kazi, ambao ni nyenzo inayowezesha kuutafsiri Mpango Kazi wa FSDMP katika ngazi ya sekta ndogo husika, hivyo kurahisisha utekelezaji wa shabaha husika zilizoainishwa kwenye FSDMP. Kwa mukhtadha huo, sekta ndogo ya bima imejiwekea Mpango kazi wake (ISAP); na ikaunda kikosi kazi cha masuala ya bima (TWG) chenye wadau mbalimbali wa sekta ndogo ya bima. TWG hufanya mikutano yake ya kawaida mara mbili kwa mwaka chini ya Uenyekiti wa Kamishna wa Bima (Afisa Mtendaji Mkuu wa

TIRA) na Makamu Mwenyekiti anatoka kwenye Umoja wa Makampuni ya Bima (ATI). Lengo kuu la TWG ni kutathmini na kutoa taarifa ya utekelezaji wa ISAP, na pia masuala mengine ya kimkakati ya soko la bima. TWG huwasilisha taarifa zake kwenye vikao vya Kamati ya Ufundi ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha inayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Tangu kuanza kwa utekelezaji wa FSDMP, TWG-Ins imeshafanya vikao kazi viwili. Lengo la taarifa hii ni kuujulisha umma kuhusu mafanikio yaliyofikiwa na masuala yaliyokubaliwa kwenye kikao cha tatu kilichofanyika tarehe 23 Machi 2023 katika ukumbi wa JNICC-Dar es Saalam.

**Mafanikio na Muhtasari wa Kikao cha Tatu cha Kikosi Kazi cha Masuala ya Bima Kilichofanyika tarehe 23 Machi 2023 jijini Dar es salaam**

Kikosi Kazi cha Masuala ya Bima kilifanya kikao chake cha tatu katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es salaam, Alhamis tarehe 23 Machi 2023. Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, uliainisha mafaniko kadhaa yaliyopatikana katika utekelezaji wa FSDMP ambayo ni pamoja na:

i. **Tasnia ya Bima kushiriki katika uchumi wa Gesi na Mafuta kwa Kuanzishwa kwa Muungano wa Kampuni za Bima za Utoaji wa Bima za Mafuta na Gesi (Oil and Gas Consortium).** Ufunguzi huu wa Bima ya pamoja ulifanyika tarehe 22 Novemba 2022 chini ya mgeni rasmi **Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Hamad Hassan Chande.**
Muungano huo ulianzishwa na kuzinduliwa mwezi Novemba 2022 ili kuweka utaratibu wa pamoja wa kampuni za bima kutoa kinga ya bima kwa majanga makubwa na maalum katika sekta ya Mafuta na Gesi; Pia kuongeza uwezo Taifa letu kubakiza (retention levels) tozo za bima na kuongeza mzunguko wa fedha nchini.

ii. **Kuanzishwa kwa aina mpya za bidhaa za bima**
Jumla ya bidhaa mpya za bima zipatazo 17 zimeanzishwa kwenye soko la bima kukidhi mahitaji ya wananchi hususan wa kipato cha chini. Bidhaa hizi ni pamoja na huduma za bima kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati na bidhaa za kilimo na uvuvi.

iii. **Uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa bima kati ya TIRA na Mamlaka zingine za Serikali**
TIRAMIS (mfumo wa TEHAMA wa bima ulioundwa na TIRA) umeunganishwa na mifumo ya Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA), Jeshi la Polisi Tanzania (TPF), na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA). Kuanzia sasa, hakuna bima ya chombo cha moto itatolewa kwa chombo cha moto bila ya uhakiki wa taarifa za chombo husika na TRA. Aidha, utoaji wa leseni za LATRA utazingatia uwepo wa bima halali na hai ya chombo cha moto husika. Uunganishwaji wa mifumo utaimarisha usimamizi wa Jeshi la Polisi wa sheria za usalama barabarani, hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa utumiaji wa vyombo vya moto visivyo na bima stahiki. Hatua hii, pamoja na mambo mengine, itaimarisha ulinzi wa haki za wanufaika wa bima na umma kwa ujumla.

iv. **Utoaji wa Miongozo Mipya ya Usimamizi wa Bima:**
TIRA imetoa Miongozo kadhaa ikiwemo Miongozo ya Maafisa Wauza Bima; Miongozo ya Utoaji wa Bima Kidijitali; Miongozo ya viwango vya kimataifa vya taarifa ya kifedha. (IFRS) 17; Miongozo ya Uendeshaji wa shughuli za Bima za Takaful; Miongozo ya Uwekezaji na Usimamizi wa Ukwasi; Miongozo ya Usimamizi wa Madai ya Bima; Miongozo ya Benkibima (Uendeshaji wa Biashara); na Miongozo ya Viwango vya Chini vya Mafao kwa Wahanga wa Ulemavu au Vifo vinavyotokana na Ajali za Vyombo vya Moto. Faida ya Miongozo yote hii ni kupanua wigo wa utoaji na upatikanaji wa huduma za Bima kwa umma; kulinda haki za wateja na kuongeza ajira rasmi na zisizo rasmi katika mnyororo wa sekta ya Bima.

v. **Uanzishwaji wa Njia Mpya za Usambazaji wa Huduma za Bima:**
Ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi, njia mpya 4 za usambazi wa huduma za bima zimeanzishwa yaani, uwakala wa benkibima, bima za Takaful, majukwaa ya utoaji wa bima kidijitali, na maafisa wauza bima.

vi. **Usambazaji wa Bima kupitia Mitandao ya Simu (MNO)**:
Ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi***,*** kampuni tatu (3) za simu zinatoa huduma za bima kwa kutumia teknolojia ya simu.

**vii Ukuaji Imara wa Soko la Bima**:
Soko la bima limeendelea kukua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 12.2 kwa mwaka kwa miaka mitano iliyopita.

**viii Kuongezeka kwa watoa huduma za Bima**
Watoa huduma wa Bima wakiwemo Makampuni ya Bima, Wataalam wa Ushauri wa Bima, Mawakala wa Bima, Wataalam wa Bima, Wataalam wa Bima Mtawanyo, Wakadiriaji hasara, Bankiwakala wa Bima, Wauza Bima Kidigitali, Wachunguzi binafsi wa Bima wameongezeka kwa asilimia 12.84% mpaka kufikia Desemba mwaka 2022.

**Ix Mchango wa Sekta ya Bima kwenye Uchumi .**
Mpaka kufikia Desemba 2022 Soko la Bima kupitia ada za ima limechangia kiasi cha Shilingi Trilioni 1.149 kwenye pato la Taifa kutoka Shilingi Bilion 912 cha desemba 2021.

**Matarajio ya Baadae ya Sekta Ndogo ya Bima**
Sekta ndogo ya bima chini ya usimamizi wa TIRA itaendelea kutekeleza shabaha mahususi zilizoainishwa katika Mpango Mkuu wa Maendeleo wa Sekta ya Fedha (FSDMP 2020/21 – 2029/30) na kwenye Sera ya Uchumi wa Bluu. Matarajio ya baadae ni kama ifuatavyo:

i. Kuanzisha kwa Skimu ya Taifa ya Kilimo (Tanzania Agriculture Insurance Scheme - TAIS);
ii. Kukamilishwa kwa Sera ya Bima ya Taifa (National Insurance Policy - NIP);
iii. Kuendelea na uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa bima kati ya TIRA na Taasisi zingine za Serikali (kama vile TASAC, TPA, NIDA, NSSF, NHIF, CHF, na WCF) ili kuongeza tija na ufanisi ndani ya sekta ndogo ya bima na pia kupunguza gharama za usimamizi;

iv. Kufanya marekebisho katika Sheria ya Bima Sura Na. 394 na Kanuni zake, pamoja na kuandaa Kanuni Mpya za Bima kwa lengo la kuboresha mfumo wa usimamizi na uendelezaji wa bima nchini; na
v. Kuanzishwa kwa Bodi ya Wataalam kwenye Tasnia za Bima, bodi hiyo itaitwa Insurance, Social Protection, and Actuarial Board – ISPAB. Lengo la bodi ni kuongeza fursa za kutambulika na tija kwa wanataaluma husika.
vi. Kukamilisha kwa Kanuni za Bima za Lazima.

TIRA kama msimamizi wa Bima inaendelea kukamilisha kanuni za Bima za lazima katika maeneo yafuatayo:
(a) Majengo ya Biashara
(b) Masoko ya Umma
(C) Bidhaa zinazotoka nje
(d) Vyombo vya Usafiri wa Majini kama vile Meli, Boti na Feri au Vivuko.

Kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Taifa ya Maendeleo ya Fedha (FSMP), TIRA inatoa wito kwa wakatabima, wanufaika wa bima na umma kwa ujumla kuendelea kutumia bidhaa na huduma za bima zinazotolewa na soko la bima la Tanzania katika kukabiliana na athari za majanga mbalimbali yanayoweza kuwatokea katika maisha yao, afya zao, mali zao na biashara zao. Mamlaka inauhakikishia umma wa Watanzania kwamba itaendelea kuendeleza na kusimamia soko la bima jumuishi, lenye ufanisi, linalozingatia haki, usalama na himilivu, soko lisilo na udanganyifu lenye kufuata weledi, ushindani na faida.

***IMETOLEWA NA MWENYEKITI WA KIKUNDI KAZI CHA MASUALA YA BIMA***

Dkt. Baghayo A. Saqware
***<u>KAMISHNA WA BIMA</u>***